RAIA MWEMA | UK 8.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Kahama Fresh, Josam Mtangeki (kushoto) akitoa maelezo kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, kuhusu mitambo iliyofungwa katika kiwanda cha kuchakata maziwa na chakula cha mifugo cha kamouni hiyo namna itakavyofanya kazi, alipokagua maendeleo ya kiwanda hicho wilayani Karagwe, Kagera juzi. (Na Mpiga Picha Wetu).

# Ndaki ahimiza wawekezaji binafsi

**Na Mbaraka Kambona, Kagera**

**WAZIRI** wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amehimiza wawekezaji wa sekta binafsi kuwekeza kwenye mifugo kuliko na fursa kubwa ya kukuza mitaji na kupata faida.

Alitoa mwito huo juzi alipokagua maendeleo ya kiwanda cha kuchakata maziwa na chakula cha mifugo cha Kahama Fresh wilayani Karagwe mkoani hapa.

Waziri Ndaki alisema uwekezaji huo unawezekana, akitolea mfano mwekezaji Kahama Fresh aliyeanza uwekezaji kwenye shamba alilopewa na Serikali na sasa ana kiwanda cha maziwa na chakula cha mifugo.

"Wizara ya Mifugo tuko tayari kumwunga mkono mwekezaji yeyote atakayewekeza kama Kahama Fresh, ili ufugaji uwe wa kibiashara zaidi na kuleta tija kwao na Taifa kwa ujumla," alisema.

Alisema wawekezaji hao binafsi wakiwekeza katika sekta ya mifugo na kufanya ufugaji wa kibiashara, watasaidia kuongeza fursa za ajira kwa wananchi, lakini pia watakuza pato la Taifa.

Aidha, alisisitiza kuwa kupitia uwekezaji wao, watasaidia wafugaji wengine wanaofanya ufugaji wa kujikimu, kujifunza kupitia kwao na kufanya ufugaji wenye tija zaidi.

Mwekezaji wa Kahama Fresh, Josam Mtangeki alisema wamekuwa wakipata changamoto ya maji na chakula cha mifugo hasa wakati wa kiangazi, hivyo kuiomba Wizara kumwongeza eneo la lisilopungua hekta 2,000 ili kulima malisho ya mifugo yake na mengine akopeshe wafugaji wadogo wanaomuuzia maziwa.

# Waziri Ndaki awaeleza wawekezaji faida za kuwekeza sekta ya mifugo

NA MBARAKA KAMBONA, KAGERA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewahimiza wawekezaji sekta binafsi nchini, kuwekeza katika sekta ya mifugo kwa sababu kuna fursa kubwa ya kukuza mitaji yao na kupata faida.

Alitoa wito huo wilayani Karagwe, mkoani hapa, juzi alipotembelea na kukagua maendeleo ya kiwanda cha kuchakata maziwa na chakula cha mifugo cha Kahama Fresh.

Ndaki aliwahimiza wawekezaji wa sekta binafsi kuwekeza sekta ya mifugo kwa sababu inawezekana, huku akimtolea mfano mwekezaji wa Kahama Fresh aliyeanza uwekezaji katika shamba alilopewa na serikali na kufungua kiwanda cha kuchakata maziwa na chakula cha mifugo.

"Niseme tu kwamba sisi Wizara ya Mifugo tuko tayari kumuunga mkono mwekezaji yeyote atakayefanya uwekezaji mahiri kama alivyofanya Kahama Fresh, ili shughuli ya ufugaji iwe ya kibiashara zaidi na kuleta tija kwao binafsi na taifa kwa ujumla," alisema.

Aliongeza kwa kusema wawekezaji hao wakiwekeza sekta ya mifugo na kufanya ufugaji wa kibiashara watasaidia kuongeza fursa za ajira kwa wananchi na kukuza pato la taifa.

Ndaki alisisitiza kupitia uwekezaji wao watasaidia wafugaji wengine wanaofanya ufugaji wa kujikimu kujifunza kupitia kwao na kufanya ufugaji wenye tija zaidi.

Mwekezaji wa kiwanda cha Kahama Fresh, Josam Mtangeki, alisema wanakabiliwa na changamoto ya maji na chakula cha mifugo hususan wakati wa kiangazi.

Kutokana na hilo, aliiomba wizara kumwongezea eneo lisilopungua hekta 2,000 la kulima malisho ya mifugo yake na mingine atawakopesha wafugaji wadogowadogo wanaomuuzia maziwa ya kuyachakata



**MKUU wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila (kulia), akizungumza na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ofisini kwake mjini Bukoba mkoani humo, juzi.** (Picha na Wizara ya Mifugo).

CamScanner

ja wa
oja na
ia za
i.
ma za
alise-
akati
mbili
firisha
ndal-
ara ya
Ofisi

wa
ote
ati wa
hakik-
kwa
epitia
ama
a na
anga
emi-

nzo ya
kali
wa
go la
aida
a
pata
ga-
eva
a

ereva
za
arishi
wa

kali inakusanya mapato yake vi-

lenga katika kubaini changamoto zinazowakabili wakati wa maku-

kwani vitasaidia kulipa kodi kwa hiari bila ya usumbufu.

katika ukusanyaji wa mapato ya serikali," alisema Badru.

HABARI LEO UK 16.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (kulia) akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Kahama Fresh, Josam Mtangeki (kushoto) kuhusu mitambo iliyofungwa katika kiwanda cha kuchakata maziwa na chakula cha mifugo cha Kahama Fresh namna itakavyofanya kazi alipokitembelea kukagua maendeleo ya kiwanda hicho kipya kilichopo wilayani Karagwe, Kagera juzi. (Picha na Wizara ya Mifugo na Uvuvi).

CamScanner

# WEEK'S EVENTS ASSORTM

DAILY NEWS Page 5.



*Minister for Livestock and Fisheries, Mr Mashimba Ndaki (left) listens to Kagera Regional Commissioner, Mr Albert Chalamila at the latter's office. The minister was on a one day working tour to inspect various activities related to livestock and fisheries sector in Kagera region. (Photo by Ministry of Livestock and Fisheries)*

CamScanner

The Guardian

# Ndaki encourages private investors in dairy farming

By Guardian Correspondent, Kagera

MASHIMBA Ndaki, Minister for Livestock and Fisheries, has encouraged investors in the private sector to invest in the livestock sector including the dairy farming due to the marvelous opportunities found on it so as to grow their capitals and earn more income.

He made the call when he visited and inspected the progress of the Kahama Fresh milk and animal feed processing plant located in Karagwe District, Kagera Region on Thursday.

Minister Ndaki cited an example of the Kahama Fresh investor who started investing in a farm given to him by the government and until now has opened a big factory to process milk and animal feed.

"Let me assure you that the ministry is here to support any investor who will be able to make a smart investment so as to promote development of the dairy sub-sector in which its market is growing locally and overseas," he said.

He added; "Investors who are interested to establish projects in the livestock sector are assured of close support from the government sector which has continued to improve key infrastructures such as roads, water and energy as well as putting other attractive business conditions to enable them operate smoothly, produce jobs and contribute in the country's economic growth."

The minister further emphasized that through their investment they will be also linked to other breeders who are doing subsistence farming to enter agreements that will stimulate production and increase income.

Josam Mtangeki, Kahama Fresh Factory investor commended the government for putting a conducive business environment but only few challenges are still thwarting their operations.

He named them as shortage of water and access to enough animal pasture especially during the summer asking the ministry to increase the area of not less than 2000 hectares to enable them cultivate pastures for livestock.